



**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**  
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz  
155 Merrimack Street  
Lowell, MA 01852

Disemba 22, 2020

Salamu Jamii ya Lowell Public Schools,

Ninatarajia kwamba barua hili litakupata wewe na familia yako mkiwa salama na wenye afya huku tukielekea kuingia sherehe za sikukuu. Hali likizo ya kipupwe ikianza mwisho wa siku ya shule Jumatano, ningependa kugawa nawe taarifa mpya kuhusu data ya COVID-19 ya eneo na namna tunavyoendelea kufuatilia data hiyo huku tukizingatia tarehe tunazoweza kuendelea na mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi darasani.

Kila Alhamisi, Jimbo huru hufunua muhtasari wake wa COVID-19 wenye msingi wa jamii. Ripoti ya mwisho kabisa inaonyesha kwamba data ya COVID-19 hapa Lowell – na kote Massachusetts – inaendelea katika mwelekeo usiofaa. Nambari ya wastani ya matukio ya maradhi ya kila siku katika wakaazi 100,000 iliongezeka kufika 134.4 na “kiwango cha asilimia cha kuwepo kwa maradhi” (asilimia ya vipimo vilivyopatikana na maradhi hapa Lowell) iliongezeka kufika 12.33%. Idadi hizi zote mbili zinazidi kwa kiasi kikubwa kiwango cha Jimbo huru linaloweke Lowell katika hali ya hatari ya juu. Ili kulinganisha, katika katikati ya mwezi wa Oktoba, kiwango cha wastani cha Lowell cha matukio ya maradhi ya kila siku kilikuwa 16.4 na asilimia yetu ya kuwepo kwa maradhi ilikuwa 3.29%. Katikati ya mwezi wa Novemba, kiwango cha wastani chetu cha matukio ya maradhi ya kila siku kilikuwa 42.1 na kiwango yetu ya asilimia ya kuwepo kwa maradhi ilikuwa 6.45%.

Afya na usalama wa wanafunzi na wafanyikazi wetu ni lazima uwe katika kipaumbele ya kila uamuzi tunaofanya, kwa hivyo **shule inapoanza upya baada ya likizo ya msimu wa kipupwe mnamo Jumatatu, Januari 4, 2021, wanafunzi wote wa Lowell Public Schools wataendelea na mafunzo ya mbali.**

Jana usiku, baada ya mashauriano na Bodi la Afya, Kamati ya shule ilipangia kulenga tarehe zifuatazo kwa wanafunzi kurejelea shuleni kuhudhuria madarasa, sharti data ya COVID-19 data iweze kuboreka kati ya sasa na tarehe hizo:

- Februari 1 – Wanafunzi katika programu za masomo maalum zilizo na tofauti kubwa na masomo ya kawaida waliokuwa wakishiriki katika mafunzo yetu ya kuhudhuria darasani hapo awali
- Machi 1 - Wanafunzi, wasio katika programu za masomo maalum zilizo na tofauti kubwa na masomo ya kawaida, lakini waliohudumiwa katika mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kama sehemu ya mpango wetu wa awali wa kufungua upya
- Aprili 1 – Kupanua muundo wetu wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kuongezea wanafunzi wa ziada zaidi ya wale walioteuliwa kuhudhuria kibinafsi mwanzo wa mwaka huu wa shule

Tarehe hizi si thabiti na tutaendelea kurejelea data ya COVID-19 na kushauriana na Bodi la Afya. Pia tutahakikisha tunakuarifu ipasavyo tunapoangazia mpango wetu wa mafunzo siku zijazo. Ingawa hatutarejea kimwili darasani kuanza mwaka wa 2021, tutaendelea kuwapatia wanafunzi wetu uzoefu wa usalama na wenye maana kwa njia ya mbali.

Kama kawaida, tafadhali usisahau kufuata itifaki za usalama zinazopunguza usambazaji wa COVID-19. Hizi ni zikiwamo umbali wa kijamii, kuvaa barakoa, kunawa mikono yako, kutokusanyika katika vikundi vikubwa, na kutogawa vyakula, vinywaji au vyombo. Kasi tunavyoboresha idadi za maradhi za COVID-19 hapa Lowell, ndiyo kasi tunayoweza kuwarejesha wanafunzi wetu shuleni.

Hii imekuwa mwaka yenye changamoto kwa watu wengi kwa sababu nyingi tofauti, kwa hivyo ninawashukuru kwa dhati kwa subira yenu, uwezo wenu wa kukubali mabadiliko kwa urahisi, na ushiriki wenu katika muda huu wote usiyowahi kuonekana awali.

Ninakutakia mwaka mpya wenye furaha na afya,

Dr. Joel D. Boyd  
Msimamizi Mkuu wa Shule